OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

SHULE YA SEKONDARI KILAMACHO
S.L.P 81,
MKUU- ROMBO
Namba ya simu: 0756 237 590, 0713 840 876.
14 - Disemba, 2020

Kumb. Na. KLMSS/JI/Vol.I/2020/16

JINA LA MWANAFUNZI:_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI KILAMACHO

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 . Hongera sana na karibu sana.

2.0 KUANZA MASOMO

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11 Januari,2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08/01/2021 SIKU YA IJUMAA ukiwa na mazazi/mlezi wako saa 2:00 asubuhi bila kukosa kwa ajili ya kuandikishwa.. Tutakuwa na kikao cha wazazi wa wanafunz iwa kidato cha kwanza 2021 siku hiyo saa tatu (3:00) asubuhi kwa ajili ya kupewa maelekezo mengine. Ukishindwa kuripoti shuleni ndani ya siku saba tangu shule kufunguliwa hatua zitachukuliwa.

3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

3.1. SARE ZA SHULE.

a) WAVULANA

i. Suruali mbili ndefu zisizobana. (za rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa)
ii. Shati nyeupe mbili za mikono mifupi ya kawaida.
iii. Sweta mbili (za rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa, mtindo wa nanasi)
iv. Viatu vya Rangi Nyeusi vya kufunga kwa kamba (epuka viatu vya kubadilisha rangi au Raba).
v. Soksi nyeupe jozi mbili.
vi. Mkanda mweusi wenye bakoli ya kawaida isiyo na picha.

b) WASICHANA

i. Sketi mbili ndefu zinazopita magoti. (za rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa)
ii. Blauzi mbili nyeupe mikono mifupi ya kawaida
iii. Soksi nyeupe jozi mbili
iv. Sweta mbili. (za rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa, mtindo wa nanasi)
v. Viatu vya rangi nyeusi vya kufunga kwa kamba (epuka viatu vya kubadilisha rangi au Raba).

*NB:**Wasiliana na mafundi mtaani,wenye uwezo wa kushona sare za shule ipasavyo wenye RANGI ya kipande cha kitambaa kilichoambatanishwa na si vinginevyo.***

3.2 SARE ZA MICHEZO:

Edit with WPS Office

i) Wavulana: Bukta na T-shirt za rangi ya bluu na viatu vya michezo rangi yeyote.

ii) **Wasichana:** Bukta na T-shirt za rangi ya bluu na viatu vya michezo rangi yeyote (trucksuit inakubalika)

3.3 VIFAA VYA KUJIFUNZIA:

- Daftari (counter book) tisa (9) za "2 quire"
- Kamusi ya kiingereza (Dictionary)
- Mkebe wa hesabu (mathematical set)
- Kalamu za wino wa bluu au mweusi, penseli, kichongeo na rula.
- Begi la kuhifadhia vifaa. (mifuko mbadala hairuhusiwi)

3.4. VIFAA VYA CHAKULA

- Kikombe, Sahani au bakuli ya bati (alluminium) na kijiko kwa ajili ya uji na chakula cha mchana.

3.5. MCHANGO WA CHAKULA:

Mchango wa Chakula uliokubalika kwenye kikao cha wazazi ni shilingi elfu 80,000/= kwa mwaka (muhula 40,000/=) Lakini viwango hivi vinaweza kufanyiwa marekebisho kuendana na bei za vyakula sokoni na maamuzi ya kikao cha wazazi.

Fedha hizo husimamiwa na kamati ambayo huteuliwa na wazazi wenyewe.

Kumbuka serikali imefuta ada na michango mingine shuleni lsipokuwa michango iliyokubaliwa na

kupitishwa na wazazi/walezi katika mikutano yao kulingana na uhitaji.

3.6 VIFAA VYA USAFI

- Fagio moja
- Ndoo moja plastic ya ujazo wa lita ishirini.
- Dekio la aina yeyote.

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara zenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu hapa nchini.

4.1 Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

i. Kuwa na heshima, utii na adabu kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.

Unapozungumza na wakubwa ni lazima ***USIMAME*** kwa adabu na uwe mtulivu. Ni kosa kuzungumza na Mkubwa au kiongozi yeyote ukiwa umeweka mikono mfukoni, unayumbayumba au kuegemea kitu kama meza, kiti au ukuta.

ii. Ukiwa darasani unatakiwa kusimama na kuamkia wakati Mwalimu au kiongozi anapoingia.

iii. Unatakiwa kuheshimu Chama kinachotawala, Serikali iliyopo madarakani, wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Picha za viongozi na Fedha (Sarafu au Noti) ya Taifa.

Edit with WPS Office

iv. Ni muhimu kuhudhuria vikao vyote halali vya shule

v. Ni marufuku kufuga ndevu (Wavulana), kuwa na kucha ndefu, kupaka kucha rangi na kubadili nywele kwa kuweka ***DAWA au kutumia vipodozi***.

vi. Ni marufuku kufika shuleni na vifaa vya muziki kama. Walkman, Redio, simu ya mkononi na Kamera. ***UKIKAMATWA NAVYO VITACHUKULIWA NA HUTARUDISHIWA KABISA***.

vii. Ni marufuku kuonekana katika sehemu zifuatazo;

a. Vilabu vya pombe

b. Majumba ya Starehe

c. Majumba ya kufikia wageni

d. Sehemu za michezo ya "Pull Table" na kamari ya aina yeyote

e. Sehemu za kuonyesha picha (video shows) na mipira ya miguu..

f. Huruhusiwi kwenda au kutembelea nyumba za watumishi wa shule bila kibali maalum.

g. Unatakiwa kuvaa ***SARE KAMILI*** ya shule muda wote utakapokuwa shuleni au unaposafiri nje ya shule.

h. Ni marufuku kutumia Lugha ya Matusi, kashfa au uongo kwa Walimu, Wafanyakazi na Wananchi ukiwa nje au ndani ya shule.

i. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza.

j. Lugha ya Kiswahili itatumika wakati wa masomo ya Kiswahili na Dini tu.

4.2 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI:

A) Wizi
B) Uasherati, ubakaji na ushoga.
C) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
D) Uvutaji wa bangi na sigara.
E) Makosa ya Jinai
F) Kupigana au kupiga
G) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
H) Kudharau Bendera ya Taifa
I) Kuoa au kuolewa
J) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
K) Kutoa mimba
L) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
M) Kukataa adhabu kwa makusudi.

4.3 Yafuatayo ni muhimu kuyazingatia;

- Kuwahi mara zote kufika shuleni/darasani
- Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku, kama vipindi vya darasani, kazi za mikono, michezo na usikose kutekeleza unayopangiwa.
- Kazi za mikono ni sehemu ya Elimu, hivyo utegaji na uzembe kamwe hautavumilika
- Lazima kuwahi katika wito unaokuhusu.
- Wakati wa masomo unatakiwa uwe darasani bila makelele au kutembeatembea.
- Kujificha sehemu yoyote wakati wengine wakiwa mstarini au darasani ni kosa.
- Ni kosa kutokufika (au kutohudhuria) darasani siku za masomo au kutoroka.

NB: Ukishindwa kuzingatia mambo haya utapewa adhabu kali.

Edit with WPS Office

5.0USAFI.

i. Unatakiwa kuzingatia sana usafi wako binafsi na mazingira unayoishi.
Ni kosa kuona na kupita karatasi au takataka bila kuziokota na kuzipeleka mahali pake na kuzichoma.

ii. Kutokushiriki kikamilifu katika shughuli za usafi wa mazingira kama utakavyopangiwa na uongozi wa shule ni kosa.

6.0 AFYA :

Hakikisha kuwa umepimwa afya yako na daktari na akujazie fomu iliyoambatanishwa. Maelekezo ya daktari yatamsaidia Mwalimu kutoa huduma inayostahili kwa mwanao.

6.1 KUKUBALI/ KUTOKUBALI

Mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi mnatakiwa kujaza fomu A ili kuonesha umekubali au umekataa nafasi hii adimu uliyopewa.

KARIBU SANA KILAMACHO SEKONDARI.

……

MKUU WA SHULE

Edit with WPS Office

“ FOMU A”

SHULE YA SEKONDARI KILAMACHO

FOMU YA MWANAFUNZI / MZAZI YA KUKUBALI

NAFASI SHULENI

A. Mimi…… (Jina la mwanafunzi)

NINAKUBALI/SIKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Kilamacho. Ninaahidi kuwa nitatii kanuni na sheria zote za shule na kufuata kikamilifu masharti yote yatakayotolewa na Mkuu wa shule au mwalimu au yeyote mwenye mamlaka shuleni. Ninaahidi pia kwamba nitajitahidi kushirikiana na wenzangu katika shughuli zote za masomo, uzalishaji mali na michezo. Na sitashabikia au kujihusisha na mambo maovu shuleni kama kuanzisha au kuchochea migomo. *DINI/* ***DHEHEBU*** langu ni …… …….(Taja kama wewe ni Mkatoliki, Mlutheri, S.D.A, Mwislamu, Pentekoste n.k)

……..

SAHIHI YA MWANAFUNZI

B. IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi) …….. wa (anwani/namba ya simu)……..

Nakubali nafasi aliyotunukiwa mwanangu ya kujiunga na SEKONDARI. Ninaahidi vile vile kuwa nitashirikiana na Mkuu wa shule na Walimu kumlea kitabia na kimasomo pia kumtimizia mahitaji yake yote ya shule na nyumbani kwa kadri itakavyohitajika. Pia nitahudhuria vikao vya wazazi shuleni au wito maalumu kwa ajili ya kupata taarifa ya maendeleo na nidhamu ya mwanangu.

……

SAHIHI Y MZAZI/MLEZI

Edit with WPS Office

"FORM B"

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be filled by medical officer from government hospital/health center)

KILAMACHO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 81,
MKUU -ROMBO.

TO MEDICAL OFFICER
REGIONAL/DISTRICT HOSPITAL/HEALTH CENTER

STUDENT'S NAME …….

REF: MEDICAL EXAMINATION

Kindly may you examine the mentioned student on his/her fitness to enable us to handle him/her according to his/her health condition.

Blood testing ……
Diagnosis ……..
HIV/AIDS ……
STI's/STD's……
TB. ……
Urine testing ……
Diagnosis ……
Ears testing ……..
Diagnosis ……
Eyes testing ……
Diagnosis ……
Any disability observed ……..
Comments/suggestion from medical officer ……
……

Name of examiner / medical officer …….

Signature ……

Official stamp …….

Edit with WPS Office